

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
SUMBAWANGA



**MKATABA MDOGO WA KAZI YA UCHIMBAJI WA
MTARO NA ULAZAJI WA MABOMBA KATIKA MANISPAA
YA SUMBAWANGA**

MKATABA HUU unafanyika leo tarehe 02 mwezi 08 Mwaka 2022

BAINA YA

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SUMBAWANGA

(SUWASA) S.L.P 192 (ambaye katika Mkataba huu atajulika na kama "Mwajiri")

NA

EMMANUEL GERAD RUCIAN (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiriwa").

KWAMBA kwa pamoja Mwajiri na Mwajiri watajulikana kama pande mbili za Mkataba.

AMBAPO:

- a) Mwajiri ni SUWASA
- b) Mwajiriwa ni EMMANUEL GERAD RUCIAN
- c) Mwajiri anakusudia kumwajiri Mwajiriwa kwa kipindi cha muda mfupi siku kumi arobaini na tisa tu.
- d) Mwajiriwa anakubali matakwa ya Mwajiri na anakubali kwa hiari yake mwenyewe kuajiriwa kwa muda mfupi.

MKATABA HUU UNASHUHUDIA kwa pande zote mbili kukubaliana kama ifuatavyo:

1. MADHUMUNI YA MKATABA

Mkataba huu ni kwa ajili ya **Uchimbaji wa Mtaru na Ulazaji wa Bomba, kwa gharama ya Tsh.1500 kwa mita moja** ambapo kwa Jumla ya Mita 14,000 Gharama itakuwa Tsh.21,000,000/=.

Mwajiriwa atapaswa kufanya kazi zifuatazo:

- a) Kuchimba mtaro urefu wenye kina cha mita moja na urefu wa mita 14,000
- b) Kulaza bomba zenye urefu wa mita 14,000
- c) Kufukia mtaro wa urefu wa mita 14,000

2. MUDA WA UTEKELEZAJIWA KAZI

Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 29, ambapo itaanza tarehe 02/08/2022 na itakamilika tarehe 31/08/2022.

3. MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI

- a) Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha Tshs. 21,000,000/= kwa ajili ya uchimba wa mtaro, ulazaji wa mabomba, na ufukiaji wa mtaro wenye urefu wa mita 14,000
- b) Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni kwa fedha za kitanzania tu (Tanzanian Shillings);
- c) Malipo hayo yatalipwa kwa hundi kwa kutumia akaunti ya Mwajiriwa
- d) Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kwa awamu mbili (4) kama ifuatavyo:
 - (i) Malipo ya awamu ya awamu ya kwanza yatakuwa Tsh. 6,750,000/= yatalipwa mara baada ya kukamilisha kazi ya kuchimba mtaro na kulaza bomba urefu wa mita 4500.
 - (ii) Malipo ya awamu ya pili yatakuwa kiasi cha Tsh.7,500,000/= ambayo yatalipwa mara baada yakukamilisha kazi ya kuchimba mtaro na kulaza bomba urefu wa mita 5000.
 - (iii) Malipo ya awamu ya pili yatakuwa kiasi cha Tsh.6,750,000/= ambayo yatalipwa mara baada yakukamilisha kazi ya kuchimba mtaro na kulaza bomba urefu wa mita 4500.
- (e) Mwajiriwa atakatwa kodi ya zuiro (*withholding tax*) ambayo ni 5% ya gharama ya kazi iliyoainishwa katika Mkataba.

4. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri ambaye atawakilishwa na Msimamizi wa Kazi, atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

- a) Kusimamia na kuthibitisha ubora wa kazi inayofanywa.
- b) Kuunga bomba kwa njia ya Moto (Fusion) na kutumia viungio/
- b) Kuwasiliana na uongozi wa eneo husika kuhusu njia ambayo Mtaru utapita.

